

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA MARA

Anuani ya Simu: "REGCOM".

Simu Nambari 028/2622004/2622005

Fax 028-2622764/2622324

E-mail: ras.mara@tamisemi.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA,

S. L. P. 299,

MUSOMA,

TANZANIA.

TAARIFA KWA UMMU

Siku ya Mazingira Duniani Kitaifa itafanyika Mkoani Mara Mjini Butiama kuanzia tarehe 01/06/2017 hadi tarehe 04/06/2017.

Maadhimisho hayo yatafunguliwa rasmi na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Mhe. January Makamba (Mb) tarehe 01/06/2017 na kufungwa rasmi tarehe 04/06/2017 na Makamu wa Rais ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan.

Maadhimisho hayo yanafanyika katika Uwanja wa Mwenge Mjini Butiama ambapo pamoja na sherehe hii kutakuwepo na Kongamano na tafrija mbalimbali kuhusiana na masuala ya Mazingira.

Aidha, jumla ya miche ya asili 1,500 inatarajiwa kupandwa kwenye misitu mbalimbali eneo la Butiama, kama ilivyo kawaida ya maadhimisho haya.

Wananchi wa mkoa wa Mara kiujumla tujitokeza kwa wingi ili kujumuika pamoja kwenye maadhimisho haya muhimu ambayo yatafanyika Mkoani Mara kwa mara ya kwanza.

Kauli mbiu ya mwaka huu ni **“Hifadhi Mazingira muhimili wa Tanzania ya Viwanda”**, ikiwa na maana ya ulinzi na uhifadhi wa mazingira nchini kuleta maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.

Faida ya maadhimisho hayo

- i. Kujengea jamii uwezo juu ya uelewa wa masuala ya mazingira na changamoto za kijamii zinazojitokeza katika utunzaji wa Mazingira.
- ii. Kuwawezesha wadau kushiriki katika fursa zinazohusiana na upandaji wa miti.
- iii. Kujadili mwendelezo wa utekelezaji wa shughuli zilizoratibiwa katika Mkoa na Wizara kuhusu namna bora ya uhifadhi wa Mazingira.
- iv. Kuelemisha wananchi kupanda miti ili kukidhi mahitaji ya Dunia kupambana na ongezeko la hewa ya Carbon dioxide (Ukaa).
- v. Kuenzi kazi zote za Baba wa Taifa Mwl. Julius K. Nyerere katika hifadhi ya mazingira.

Ziara rasmi ya Makamu wa Rais Mkoani Mara

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, anatarajia kufanya ziara rasmi ya siku tatu kuanzia tarehe 05 Juni, 2017 Mkoani Mara.

Mhe Samia atatembelea Wilaya ya Tarime, katika Kituo cha Afya cha Nyamwaga kinachojengwa na wananchi kwa msaada wa Mgodi wa Acacia North Mara.


Pia, Mhe. Makamu wa Rais atatembelea Bonde la Mto Mara kunakokusudiwa kuanza kilimo cha miwa na ujenzi wa kiwanda cha sukari. Mchana siku hiyo hiyo atafanya mkutano wa hadhara katika Kijiji cha Bisarwi; katika eneo hilo kunakusudiwa kujengwa kiwanda cha sukari.

Tarehe 6/6/2017 Mhe. Makamu wa Rais amepangiwa kwenda Wilaya ya Serengeti ambapo ataweka jiwe la msingi katika Hospitali ya Wilaya; mchana atafanya Mkutano wa Hadhara katika Uwanja wa Mbuzi, Mugumu Mjini.

Tarehe 7/6/2017 Mhe. Makamu wa Rais atakuwa Musoma ambapo ataweka jiwe la msingi kwenye barabara ya km.9.9 inayojengwa kwa kiwango cha lami katika Manispaa ya Musoma. Pia atatembelea kiwanda cha Samaki cha Musoma Fish Processors (T) Ltd.

Aidha, Mhe. Makamu wa Rais atafanya Mkutano wa Hadhara katika uwanja wa Mkendo Musoma Mjini. Hii ni mara ya kwanza Makamu wa Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan kuwa na ziara rasmi Mkoani Mara.

Imetolewa na,



Jamal Zuberi
Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano
Mkoa wa Mara.